

**TAARIFA YA UJENZI WA MRADI WA MAJI KATIKA MJI WA KALIUA
ILIYOTOLEWA NA MKURUGENZI MTENDAJI WA TUWASA ENG. MAYUNGA
KASHILIMU KWA WAZIRI WA MAJI MHE: JUMAA H. AWESO (MB) TAREHE
29/07/2023**

Mhe. Mgeni Rasmi, Waziri wa Maji.

Kwanza kabisa nachukukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kukubali kwako kuja kutembelea na kuweka jiwe la msingi kwenye mradi huu wa maji katika Wilaya ya Kaliua. Sote tunafahamu jinsi ulivyo na majukumu mengi ya Wizara na ya jimbo lako la Pangani, lakini umetupa heshima ya pekee na sisi tunashukuru sana.

Mhe. Mgeni Rasmi, Waziri wa Maji.

Wilaya ya Kaliua ina jumla ya wakazi 678,447 (Sensa 2022) ambapo wakazi 61,406 wanaishi mjini na wakazi 617,041 wanakaa Vijijini. Mahitaji ya maji kwa eneo la Mjini ni lita 1,535,150 kwa siku na Vijijini ni lita 15,426,025 kwa siku. Hali ya upatikanaji wa maji mjini ni 44% na Vijijini ni 49%. Kwa ujumla, hali ya upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Kaliua ni 47%.

Mhe. Mgeni Rasmi, Waziri wa Maji.

Ujenzi wa mradi wa maji katika mji wa Kaliua ni sehemu ya mkakati wa Serikali kuitia Wizara ya Maji katika kuboresha upatikanaji wa huduma za Maji Safi na Salama kwa Wananchi waishio Mijini na Vijijini.

Mkataba wa ujenzi wa mradi huu ulisainiwa tarehe 16 Mei, 2022 kati ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora (**TUWASA**) na Mkandarasi **KIMUA COMPANY LTD** wa Dar es Salaam kwa gharama ya **TSh. 503,112,445.22** na utakamilika mwezi Agosti, 2023.

Mhe. Mgeni Rasmi, Waziri wa Maji.

Utekelezaji wa Mradi huu unahusisha kazi zifuatazo; Ununuzi wa mabomba na Viungio vyake, ulazaji wa bomba wenyе urefu wa km 13.5, Ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 50,000 na *mhimili* wake wa mita 12, Ujenzi wa *chemba 8* na uunganishaji wa wateja wapya 110. Lengo ni kuhakikisha Wananchi wa Kaliua Mashariki, Kaliua Magharibi na Kawawa wanapata huduma ya maji safi na salama katika umbali usiozidi mita mia nne (400m) kama inavyobainisha sera ya maji ya mwaka 2002.

Aidha, mradi huu utapunguza muda wa kutafuta maji kwa wakazi wa mitaa ya Kaliua Mashariki, Kaliua magharibi na Kawawa vilivypo kwenye Kata ya Kaliua na Ufukutwa.

Mhe. Mgeni Rasmi, Waziri wa Maji.

Kukamilika kwa Mradi huu kutaongeza Uzalishaji wa maji kutoka lita 516,000 hadi lita 566,000 kwa siku ambayo inatoka asilimia 44% hadi kufikia 50% ya mahitaji ya Maji ya Mji wa Kaliua kwa sasa wenyewe jumla ya watu 61,406 (sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022). Hadi sasa kiwango cha utekelezaji wa mradi umekamilika kwa asilimia 93.

Mhe. Mgeni Rasmi, Waziri wa Maji.

Ili kuhakikisha Wilaya ya Kaliua inapata maji ya kutosheleza mahitaji ya sasa na yajayo hadi mwaka 2040, Wizara ya Maji imeanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji ya ziwa Viktoria kutoka Tabora kuititia Urambo hadi Kaliua. Mradi huu utakamilika mapema mwezi Oktoba, 2025 na utahudumia maeneo ya Vijijini na Mjini. Mkandarasi *Megha Infrastructure company limited* kutoka India tayari yuko *site* anaendelea na kazi. Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha upatikanaji wa maji kutoka 50% hadi zaidi ya 95% kwa mji wa Kaliua.

Mhe. Mgeni Rasmi, Waziri wa Maji.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (TUWASA), tunaishukuru sana Wizara ya Maji kwa kutuamini na kutupa kazi ya kusimamia mradi huu. Aidha, tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za ujenzi wa mradi huu (shilingi 503mil) ili kuendelea kuwatua akina mama ndoo vichwani.

Mhe. Mgeni Rasmi, Waziri wa Maji.

Kwa heshima na taadhima, naomba nikukaribishe sasa ukague maendeleo ya ujenzi wa mradi huu, utoe maelekezo na ukiridhia uweke jiwe la msingi kwenye mradi huu.

Karibu sana Mhe. Waziri